



TAARIFA KWA UMMA, JUMAPILI 13/06/2010

Je, wabunge wataendelea kupitisha bajeti bila kuzingatia ufanisi?

Kama wabunge hawana mamlaka ya kubadilisha bajeti iliyosomwa kwa namna yoyote, kama hawapati vitabu vya bajeti katika muda muafaka na kama wanapewa bajeti ya jumla ya serikali kuidhinisha, basi mchakato mzima wa bajeti hauzingatii ufanisi.

Kama ilivyoeleza Katiba ya Jamhuri ya Muungano, kifungu cha 90.2 (b) wabunge hawana nguvu ya kuilazimisha serikali kufanya mabadiliko yoyote katika bajeti isipokuwa kama wanataka Raisi avunje Bunge. Hii inamaanisha kwamba ifikapo tarehe 14 mwezi huu, bunge liwe limepitisha bajeti iliyosomwa na Waziri wa Fedha tarehe 10/06/2010 au bunge livunjwe kabla ya kumaliza muda wake.

Kufuatia kupitishwa kwa bajeti, Sikika inatoa wito kwa wabunge kurudi majimboni kwao kwani majadiliano ya bajeti za kisekta hayatakuwa na tija kwani hayatapelekea kubadilisha bajeti kwa namna yoyote kwani bajeti itakuwa imeshapitishwa. Kwa maana nyingine, majadiliano yote ya bajeti baada ya tarehe 14 yataongeza matumizi ambayo si ya lazima ya fedha za walipa kodi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 96 cha Kanuni za kudumu za Bunge (Toleo la 2007) Wabunge wanatakiwa kupatiwa nakala za makadirio ya bajeti ya serikali siku 21 kabla bunge la bajeti kuanza. Tunaelewa kuwa hadi kufikia tarehe 8 mwezi huu ambapo vikao vya bunge vilianza, wabunge walikuwa hawajapata vitabu vya bajeti. Je, wabunge walijiandaa vipi kujadili hotuba ya bajeti?

Vitabu vya bajeti vinatoa bajeti ya jumla ya serikali. Maelezo juu ya makadirio haya hutolewa katika vitabu vya Mpango wa kati wa matumizi ya serikali (MTEF). Kwa kawaida vitabu hivi huwa havitolewi kwa wabunge. Hii inamaanisha kwamba, kwa namna moja ama nyingine, wabunge wanapitisha matumizi bila kuwa na maelezo ya kutosha juu ya nini serikali imepanga kutumia.

Hivyo, Sikika inaona kuwa, majadiliano ya bajeti yanayoendelea hayana tija katika bajeti ya serikali na gharama za kuwaweka wabunge Dodoma ni kuongeza matumizi yasiyo ya lazima. Hivyo basi, wabunge warudi majimboni kwao kwa sababu hawana mamlaka ya kubadilisha kiasi chochote cha cha fedha kilichopo katika bajeti iliyosomwa, hawakupewa vitabu siku 21 kabla ya bunge kuanza na pia wamesomewa bajeti ya jumla ili waipitishwe.

Imetolewa na

Mr Irenei Kiria

Executive Director of Sikika, P.O.Box 12183 Dar es Salaam,
Tel: +255 222 666355/57, Fax: 2668015, Email:info@sikika.or.tz , Website: www.sikika.or.tz